# 34 Hadithi

# MIKOSI NA DHANA NJEMA

Kutoka kwa anas bun maali (Radhi za Mwenyezi ziwe juu yake), Kutoka kwa Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake), amesema:

1. "Hakuna a'd-waa, yaani maambukizi
2. Wala twiyara, yaani kuitakidi mikosi
3. Na ninafurahishwa fa-lu" wakasema: fa-lu ni nini? Akasema: "ni neno zuri" imepokelewa na Bukhari Na Muslimu [1].

1 Al-Bukhari (5776) na Muslim (2224).

## Ayah

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu

- *﴿wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizo﴾. [Al-Baqarah: 195].*
- *﴿Likiwafika jema wakisema: Haya ni haki yetu. Na likiwafika ovu husema: Musa na walio pamoja naye ni wakorofi. Hakika ukorofi wao huo unao wafikia unatoka kwa Mwenyezi Mungu. Lakini wengi wao hawajui﴾ [Al-A'raf: 131].*
- *﴿Sema: Halitusibu ila alilotuandikia Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mola wetu Mlinzi. Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu!﴾ [At-Tawbah: 51].*
- *﴿Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika Kitabu kabla hatujauumba. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi﴾. [Al-Hadid: 22].*

## Msimulizi

Ni baba Hamza, au baba Thumamah, Anas bun Malik, ukoo wa Annadhwari, Answari(ni katika waislaam walio mpokea Mtume Madina) amezaliwa miaka kumi kabla ya Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) kuhamia Madina, alikuwa ni mtumishi wa Mtume mara tu alivyoingia Madina, na Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alimuombea dua ya kujaliwa watoto wengi, mali, umri mrefu na kusamehewa dhambi. Akawa ana watoto wengi na mali, na alikuwa ni swahaba wa mwisho kufariki kwa walio kuwa katika mji wa Basra. Amefariki mwaka (93H) [1].

## Muhtasari

Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) anasahihisha itikadi ya Umma wake kwa sababu ya yaliyo kuwa yamewaathiri kabla hawajawa waislam. Akasema kwamba, maradhi kama maradhi hayaambukizi, bali hilo linatokea kwa kutaka Mwenyezi Mungu Mtukufu. na akazuia kuitakidi mikosi kwa sababu ya muda au sehemu au watu fulani, na akasema kwamba inapendeza mtu kuwa na zana nzuri kwa kusema maneno mazuri.

1 Rejea yake ufafanuzi wake katika: "Maarifaat al-Sahaba" na Abu Nu'aym (4/1846), "aliastieab fi maerifat al'ashabi"na Ibn Abd al-Bar (4/1770), "Asad al-Ghaba" na Ibn al-Atheer (3/357), "Al-Isbah fi Tamazu al-Sahaba" cha Ibn Hajari Asqalani (4/267) .

# Ufahamu

Mwenyezi Mungu Mtukufu amemtuma Nabii Muhammad (Rehma na Amani ziwe juu yake) ili awalinganie watu wamuabudu yeye pekee, na awaondolee uchafu na itikadi potofu walizokuwa nazo kabla hawajawa waislam, na hadithi hii anabainisha baadhi yake.

1 Hakuna a'd-waa, yaani maambukizi: maana yake ni msinasibishe suala la maradhi kutoka kwa mgonjwa kwenda kwa mzima kwa sababu ya kuchanganyika ni la maradhi yenyewe.

Hadithi haikanushi maambukizi, bali inakanusha suala la maradhi kama maradhi ndio yanaweza kuambukiza, bali athari zinatokea kwa mipango yake Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa ushahidi kwamba akitaka yanahama maradhi kutoka kwa mgonjwa kwenda kwa mzima kwa kuchanganyikana, na akitaka halitokei, na ushahidi mwingine ni mgonjwa wa kwanza aliugua bila kuambukizwa. Mwislam ameamrisha kuchukuwa tahadhari zenye manufaa na zinazoweza kusababisha madhara, ndio maana Mtume akaamrisha kuchukua tahadhari ili kuokoka na kujiweka mbali na walioathirika na maradhi ya kuambukiza, akasema (Rehma na Amani ziwe juu yake): "ukimbie ukoma kama unavyomkimbia simba"[(1)]. Na akasema S.A.W: "mkisikia twaa'uun (ni aina ya maradhi ya mlipuko) ardhi fulani, basi msiende katika ardhi hiyo, na ikilipuka katika ardhi mliyopo, basi msitoke ardhi hiyo" imepokelewa na Bukhari Na Muslimu[(2)]. Na akasema (Rehma na Amani ziwe juu yake): "mgonjwa hawezi kumuambukiza mzima"[(3)]. Yaani, maradhi hayaji kwa mtu ambaye ni mzima ikiwa ndio sababu ya kusambaa. Muumini anajumuisha baina ya tahadhari kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu: "wala msijitie kwa mikono yenu katika maangamizo. [Al-Baqarah: 195]. na baina ya itikadi ya kwamba mwanadamu hapatwi ila alilomuandikia Mwenyezi Mungu, kama alivyosema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Sema: Halitusibu ila alilo tuandikia Mwenyezi Mungu. Yeye ndiye Mola wetu Mlinzi. Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu! [At-Tawbah: 51].

1 Al-Bukhari (5707), kutoka kwa Abu Hurairah.

2 Al-Bukhari (5728) na Muslim (2218), kutoka kwa Usama bin Zaid, Mungu awe radhi nao.

3 Muslim (2221), kutoka kwa Abu Hurairah.

2 Hakuna Twiyara; yaani, kuitakidi mikosi, kwa sababu ya kuona au kusikia kitu fulani, mfano mtu akitaka kusafiri akaona kunguru au akasikia tukio la ajali au kifo au mfano wa hayo, akaona safari yake ina mkosi, na likamfanya asisafiri, au akasafiri akiwa na wasiwasi.

Iliitwa hivyo (twiyara-ndege), kwa sababu wasio kuwa waislam walikuwa wanaitakidi kwamba, ndege zina mikosi, walipokuwa wanataka kusafiri, wanaenda kufukuza ndege, ikirukia upande wa kulia, wanaitikidi kwamba safari ni nzuri na wanasafiri, na akirukia upande wa kushoto, wanaitakidi kwamba, safari ina mkosi na wanaiahirisha. Walikuwa wana itakidi mikosi kwenye ndege maalum, kama bundi na kunguru.

Anapolia kunguru juu ya paa la nyumba, wanadai kwamba anatoa taarifa ya kifo, na wanaitakidi mikosi, na ndio maana Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) akasema: “hakuna twiyara yaani maambukizi, wala a’d-waa, yaani kuitakidi mikosi kwenye ndege, wala haammah, wala Swafa”[1].

Haammah: ni ndege ambaye wanaitakidi kuwa ana mikosi. Na Swafar: ni mwezi wa pili katika kalenda ya kiislamu, walikuwa wakiitakidi kuwa una mikosi.

3 Kisha Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) akabainisha itikadi na dhana nzuri ni kusema maneno mazuri ambayo akiyasikia mtu anafurahi, mfano mtu akifanya kazi nzuri mwenzake akamuita “barikiwa”, na mfano wake.

Neno zuri linaifurahisha nafsi, kufungua kifua na kumchangamsha mtu, ndio maana Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) anafurahia kusikia maneno mazuri, kwa sababu si ushirikina na wala hayadhoofishi Imani katika moyo, na hata alivyokuja Suhail bun Amri kwa Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) siku ya vita ya Hudaibiya kujadili kuhusu suluhu, alifurahi na kutarajia kheri, akasema: “Mambo yenu yamekuwa mepesi”[2].

1 Al-Bukhari (5757), na Muslim (2220), kutoka kwa Abu Hurairah

2 Tazama: “Imti’ al-Asma’” cha al-Maqrizi (12/175), “Subl-Huda wa al-Rashad” cha al-Salihi (5/48).

# Mafunzo

1. Mwislam inatakiwa awe na nafsi yenye nguvu, awe na juhudi kufanya mambo ya kheri, mambo yote yanajiri kama alivyopanga Mwenyezi Mungu Mtukufu, jukumu la mwanadamu ni kufanya na kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu.

2. Ni sheria kuchukua tahadhari ambazo ni sababu za kumkinga mwanadamu dhidi ya maradhi, na wala haipingani na imani yakinifu ya kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu, linalompata, isingewezekana kumkosa. Inatakiwa muislam atekeleze wajibu wake, na atambue kwamba kila jambo liko katika mkono wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

3. Kumtegemea Mwenyezi Mungu kuliko kwa kweli, ni kuridhia na kujisalimisha kwa kutekeleza aliyoamrisha, amesema Bishru Al-haafii -Mwenyezi Mungu amrehemu-: mtu anasema: “Nimemtegemea Mwenyezi Mungu, kumbe anamdanganya! Lau angelimtegemea, angeliridhia anayoyatenda[1].

4. Inapotokea magonjwa ya mlipuko, kama Twaa’uun (ni aina ya maradhi ya mlipuko) inatakiwa mwanadamu asitoke, asiende sehemu iliyoathirika, na wala asitoke sehemu iliyoathirika, na ajisalimishe kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kutoka kwa Aisha (Radhi za Mwenyezi ziwe juu yake), hakika alimuuliza Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) kuhusu Twaa’uun, Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) akamwambia: “hiyo ilikuwa ni adhabu, Mwenyezi Mungu anaishusha kwa anaowataka, lakini akaifanya kuwa ni rehema kwa waumini, hakuna mja yeyote ambae Twaa’uun ikatokea, akabaki katika taifa lake hali ya kuwa na uvumilivu, akitambua kwamba, hakuna litakalo mpata ila alilo muandikia Mwenyezi Mungu, malipo yake ni sawa na aliyekufa akiipambania dini ya Mwenyezi Mungu”[2].

5. Kama alivyoamrisha Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) kuchukuwa tahadhari dhidi ya maradhi yenye kuambukiza, pia ameamrisha mwanadamu achukue tahadhari dhidi ya tabia mbaya ambazo mwenye nazo humuathiri aliye karibu naye. Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) amezuia kuwa na marafiki wabaya, akamfananisha rafiki mbaya na mfua vyuma, akasema: “mfano wa rafiki mbaya na mzuri, ni mfano wa mbeba miski na mfua vyuma, mbeba miski; ima akupatie au akuuzie au upate kwake harufu nzuri, na mfua vyuma; ima achome nguo zako, au upate harufu mbaya”[3]

---

1 “Madarij al-Salikeen” cha Ibn al-Qayyim (2/ 114).

2 Al-Bukhari (5734).

3 Al-Bukhari (5534), na Muslim (2628), kutoka kwa Abu Musa Al-Ash’ari

6 Miongoni mwa desturi za baadhi ya jamii ni kuitakidi mikosi katika baadhi ya wanyama, au vitu flani, au namba, au matukio fulani, itikadi hizo zinaweza kuenea katika jamii ya kiislam kwa kupitia filam na visa, Shetani anaweza kuingiza wasiwasi katika nafsi ikitokea tukio linalo amabatanishwa na itikadi hizo, kwa mwenye akili achukue tahadhari itikadi kama hizi zisienee katika jamii.

7 Kuitakidi mikosi, kama inavyopingana na kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, kuamini mipango na maamuzi yake, pia ni shari inayousababishia moyo maradhi, na kumzuia mwandamu kufanya mambo yake. Hata kama isipo mzuia, itamfanya awe na wasiwasi, akili yake haitatulia na kuamini kwamba, hakuna litakalo mpata ila alilomuandikia Mwenyezi Mungu Mtukufu, tiba yake ni kupuuzia, na kuujaza moyo kuwa na imani na Mwenyezi Mungu Mtukufu na kujisalimisha kwake, lakini pia aendelee na alichokiazimia.

8 Inaweza tokea kwa mwanadamu kuitakidi mkosi kwa sababu fulani bila kukusudia, mtu kama huyu halaumiwi ila akiridhia na kuendekeza. Amesema Ibn Masood (Radhi za Mwenyezi ziwe juu yake): “Twiyara yaani kuitakidi mikosi ni ushirikina, na hakuna kati yetu aliyesalimika, lakini Mwenyezi Mungu anaiondoa kwa Tawakkul”[1]. yaani kumtegemea Mwenyezi Mungu

9 Inatakiwa muislam awe na dhana nzuri anaposikia neno zuri, mfano mtu akimwambia: bishara nzuri, au akasikia jina zuri. Dhana nzuri hazizuii alilolipanga Mwenyezi Mungu Mtukufu, ila linaipatia nafsi raha na uchangamfu, Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alikuwa anafurahi anapo sikia neno zuri.

**Amesema haafidh al-hakamiy Mwenyezi Mungu amrehemu:**

*Kila kitu ni kwa mipango na maamuzi ya Mwenyezi Mungu ***na kila kitu kimeandikwa katika Lauhul mahfuudh (palipo andikwa mambo yote yanayotokea)*

*Hakuna kuitakidi mikosi kwenye nyota na ndege, wala hakuna kuambukiza***wala ujanja kwa lolote ambalo ameliamua Mwenyezi Mungu.*

*Wala itikadi za mikosi kwa ndege wala miezi***kama alivyo tufundisha mbora katika wanadamu*

1 Ahmad (3687).

